



BENKI KUU YA TANZANIA
— 1966-2026 —



Tathmini Ya Mwenendo Wa Uchumi

Mei 2026

Yaliyomo

1.0	Mwenendo wa Uchumi wa Dunia.....	1
2.0	Mwenendo wa Uchumi wa Taifa.....	3
2.1	Mfumuko wa Bei.....	3
2.2	Sera ya Fedha.....	5
2.3	Viwango vya Riba.....	7
2.4	Masoko ya Fedha.....	7
2.5	Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.....	9
2.6	Mwenendo wa Deni la Taifa.....	9
2.7	Mwenendo wa Sekta ya Nje.....	11
3.0	Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar.....	14
	Viambatisho.....	18



1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliingia katika robo ya pili ya mwaka 2026 ukiwa na hali ya uthabiti, licha ya kuwepo kwa vihatarishi vya kijiopolitiki, shinikizo katika masoko ya nishati, pamoja na kupungua kwa biashara za kimataifa (Kielelezo 1.1a na 1.1b). Taarifa ya hali ya uchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa toleo la Aprili 2026 na ile ya Benki ya Dunia kuhusu matarajio ya hali ya uchumi wa dunia toleo la Mei 2026, zinaonesha kushuka kwa matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia¹, licha ya kuimarika kwa soko la ajira, mahitaji ya walaji na uwekezaji katika akili unde. Aidha, mvurugiko wa mnyororo wa ugavi katika soko la nishati unaendelea kupunguza kipato halisi cha kaya, kuathiri matumizi binafsi na uwekezaji wa wafanyabiashara. Mwelekeo wa matarajio ya ukuaji unaathiriwa zaidi na hali ya migogoro ya kijiopolitiki, hususan katika eneo la Mashariki Kati.

Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia



Chanzo: <https://www.policyuncertainty.com/trade>

¹ Ripoti ya Shirika la Fedha la Kimataifa toleo la Aprili 2026 inaonesha kuwa ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.1 mwaka 2026, kutoka makadirio ya asilimia 3.3 yaliyotolewa Januari 2026. Vivyo hivyo, ripoti ya Benki ya Dunia ya Mei 2026 inaonesha ukuaji unatarajiwa kushuka hadi asilimia 2.5 mwaka 2026, ikilinganishwa na maoteo ya Januari 2026.

Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani



Chanzo: <https://worlduncertaintyindex.com/>


Mwenendo wa soko la bidhaa duniani uliakisi matokeo ya jumla ya mashinikizo ya kijiopolitiki. Mwezi Aprili 2026, bei za mafuta ghafi ziliongezeka kwa kasi, kutoka wastani wa dola za Marekani 95.58 kwa pipa mwezi Machi 2026 hadi dola za Marekani 103.91 kwa pipa, wakati bei ya juu ndani ya mwezi Aprili 2026 ikifikia dola za Marekani 117.80 kwa pipa. Mabadiliko haya, kwa kiasi kikubwa yalitokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi, hali iliyotokana na kuathirika kwa uwezo wa uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa ya mafuta ghafi. Athari za ongezeko la bei za nishati zilisambaa katika masoko mengine. Bei ya mafuta ya mawese iliongezeka, ikichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya biodizeli kutokana na kupanda kwa gharama za mafuta. Vilevile, bei za mbolea, hususan DAP na UREA, ziliongezeka kufuatia ongezeko la gharama za gesi asilia, ambayo ni malighafi muhimu katika uzalishaji wake (Kielelezo 1.2).

Kwa upande wa bidhaa za chakula, bei zilikuwa na mwelekeo mchanganyiko. Bei ya ngano ilibakia juu kutokana na hali mbaya ya hewa katika nchi zinazozalisha kwa wingi, wakati bei ya sukari ilishuka kufuatia matarajio ya mavuno makubwa nchini Brazil na Thailand, ambazo ni wazalishaji wakubwa



duniani. Aidha, bei za kahawa za Arabika na Robusta zilipungua kutokana na kuimarika kwa hali ya ugavi duniani, ikichangiwa na matarajio ya uzalishaji mkubwa nchini Brazili na Vietnam. Wakati huo huo, bei ya dhahabu ilipungua, na kubaki kufikia wastani wa kati ya dola za Marekani 4,522.1 na dola za Marekani 4,870.5 kwa wakia, kufuatia kuongezeka kwa viwango vya mapato ya hati fungani za Marekani pamoja na kuimarika kwa thamani ya dola ya Marekani, hali iliyopunguza ununuzi wa dhahabu kama hifadhi salama ya thamani. Kwa ujumla, mienendo hii ya bei za bidhaa inaashiria kuongezeka kwa gharama za uagizaji bidhaa kutoka nje, hususan kwa nchi zinazoagiza bidhaa za mafuta, chakula, na pembejeo za kilimo (Kielelezo 1.2 na Kiambatisho A8).

Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia




Chanzo: <http://www.worldbank.org/prospects>
 Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

Sambamba na mwenendo wa bei za bidhaa, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka, huku marudio ya maoteo yakifikia asilimia 4.4 mwaka 2026, kutoka asilimia 3.8 ya maoteo yaliyotolewa mwezi Januari 2026². Mwezi Aprili 2026, mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea, uliongezeka (Kielelezo 1.3), ukichangiwa zaidi na mabadiliko ya bei za nishati na kupanda kwa gharama za uagizaji bidhaa; hali iliyopelekea Benki Kuu za nchi hizo kutekeleza sera ya fedha ya kulegeza kwa tahadhari, kinyume na

liyotarajiwa mwanzoni mwa mwaka 2026. Nchi zinazoibukia kiuchumi, zilikuwa na mwenendo tofauti wa mfumuko wa bei (Kielelezo 1.3). Nchini China, mfumuko wa bei ulipungua ukichangiwa na kupungua kwa uhitaji wa ndani (*domestic demand*) na hatua za serikali za kudhibiti bei za mafuta, pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa katika sekta ya mali isiyohamishika. Nchini India, mfumuko wa bei uliongezeka kwa kiwango cha wastani, ukichochea na kupanda kwa gharama za nishati pamoja na athari zake kwenye bei za vyakula. Nchini Brazili, mfumuko wa bei uliongezeka, ukichangiwa na kuongezeka kwa gharama za pembejeo za kilimo pamoja na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Brazili (Real) dhidi ya dola ya Marekani.

Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi




Chanzo: Bloomberg

Kwa nchi nyingi Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei uliendelea kubaki ndani ya viwango vya kisera vya nchi husika (Kielelezo 1.5). Hali hii imechangiwa na hatua za awali za utekelezaji wa sera ya fedha ya kubana, kuimarika kwa viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, pamoja na utulivu wa bei za ndani za vyakula. Hata hivyo, ongezeko kubwa la bei za mafuta na mbolea katika soko la dunia linaashiria hatari kubwa ya kupanda kwa mfumuko wa bei katika ukanda huu, hususan kwa nchi zinazoagiza bidhaa hizo kutoka nje.

²Ripoti ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Aprili 2026, kusuhi Mtazamo wa Uchumi wa Dunia.




Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei kwa mwezi Aprili 2026 uliongezeka, ingawa ulibakia ndani ya wigo wa lengo la kitaifa na vigezo vya mtangamano wa kikanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Mfumuko wa bei uliongezeka hadi kufikia

asilimia 4.0 mwezi Aprili 2026 kutoka asilimia 3.2 mwezi uliotangulia, sawia na kiwango hiko katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1). Ongezeko hili limechangiwa na athari za kupanda kwa bei za mafuta, kutokana na mgogoro ya kijiopolitiki unaoendelea Mashariki ya Kati. Mfumuko wa bei kwa kipindi cha muda mfupi unatarajiwa kuendelea kukabiliwa na vihatarishi kutoka nje. Hata hivyo, kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula, utulivu wa thamani ya shilingi, na ruzuku za Serikali kwenye mafuta na mbolea, kwa pamoja vinatarajiwa kupunguza kwa kiasi athari za kiuchumi dhidi ya shinikizo kutoka nje.

Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei


2020 = 100

Makundi Makuu ya Fahirisi	Badiliko la Mfumuko wa Bei (Asilima)						
	Badiliko Mwezi hadi Mwezi			Badiliko kwa Mwaka			
	Mizania	Apr-25	Mac-26	Apr-26	Apr-25	Mac-26	Apr-26
Vyakula na vinywaji baridi	28.2	0.7	1.8	0.9	5.3	5.5	5.7
Vinywaji vikali na tumbaku	1.9	0.1	0.1	0.3	3.4	2.1	2.3
Nguu, mavazi na viatu	10.8	0.0	0.5	0.3	2.0	1.3	1.6
Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo	15.1	0.8	0.7	0.9	3.8	1.6	1.7
Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi	7.9	0.2	0.1	0.4	2.3	2.3	2.6
Alya	2.5	0.2	0.4	0.6	1.5	1.1	1.6
Usafiri	14.1	0.4	0.5	5.2	2.1	4.2	9.2
Habari na mawasiliano	5.4	0.0	0.0	0.0	0.1	1.0	1.0
Burudani, michezo na utamaduni	1.6	0.1	0.1	0.3	1.7	0.6	0.7
Elimu	2.0	0.0	0.6	1.6	4.1	0.9	2.6
Migahawa na huduma za melazi	6.6	0.3	0.4	0.1	1.6	2.1	1.8
Bima na huduma za kifedha	2.1	0.2	0.1	0.0	0.8	0.3	0.1
Huduma binafsi, hifadhi ya jamii na bidhaa na huduma mchanganyiko	2.1	0.1	0.3	0.2	3.0	3.3	3.5
Fahirisi bidhaa zote	100.0	0.4	0.8	1.3	3.2	3.2	4.0
Makundi mengine teule							
Fahirisi ya bidhaa za msingi	73.9	0.2	0.3	1.1	2.2	2.2	3.1
Fahirisi isiyojumuisha fahirishi za bidhaa za msingi	26.1	1.0	2.3	1.7	5.7	5.6	6.3
Fahirisi za mafuta, nishati na bili za maji	5.7	1.9	2.1	5.1	7.3	2.1	5.3
Fahirisi za huduma	37.2	0.2	0.3	1.8	1.1	2.4	4.0
Fahirisi za bidhaa	62.8	0.5	1.2	1.0	4.3	3.6	4.0
Fahirisi za bidhaa na huduma za elimu	4.1	0.0	0.5	0.7	3.8	0.7	1.4
Fahirisi za bidhaa zote isipokuwa chakula na vinywaji visivyo na kilevi	71.8	0.3	0.4	1.5	2.3	2.1	3.3

Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.



Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi³, uliongezeka kufikia asilimia 3.1 mwezi Aprili 2026, kutoka asilimia 2.2 katika mwezi uliotangulia na mwezi kama huo mwaka 2025 (Kielelezo 2.1.2 na Jedwali 2.1.1). Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei za usafirishaji, samani, vifaa vya nyumbani na matengenezo ya kawaida ya nyumba.

Kielelezo 2.1.2: Viwango vya Mfumuko wa bei kwa Miezi Kumi na Mbili




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa chakula uliongezeka na ulifikia asilimia 5.7 mwezi Aprili 2026 kutoka asilimia 5.5 na asilimia 5.3 ya mwezi uliotangulia na mwezi kama huo mwaka 2025 mtawalia. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei za ngano, mchele na mahindi (Kielelezo 2.1.3a, na Kielelezo 2.1.3b). Mfumuko wa bei za chakula unatarajiwa kupungua, ukichangiwa na msimu wa mavuno unaotarajiwa kuanza mwezi Mei 2026 katika maeneo mengi nchini.

³Usiojumisha vyakula visivyochakatwa, nishati na huduma za msingi zenye mabadiliko ya bei ya mara kwa mara


Kielelezo 2.1.3: Mabadiliko ya Mwaka ya Bei za Jumla za Mazao

a. Mazao ya Vyakula Vikuu



Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

b. Mazao ya Vyakula Mbadala



Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Hali ya upatikanaji wa chakula kwa ujumla iliendelea kuwa ya kuridhisha, ikichangiwa na kiasi cha akiba ya kutosha ya chakula iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Mwishoni mwa mwezi Aprili 2026, akiba ya chakula ilikuwa tani 500,962.3 ikilinganishwa na tani 533,634 katika mwezi uliotangulia, kufuatia mauzo ya tani 32,672.05 za mahindi kwa wafanyabiashara mbalimbali (Jedwali 2.1.2). Ingawa akiba ilipungua uzaji ulisaidia kuleta utulivu wa bei za rejareja, na hivyo kupunguza kasi ya ongezeko la bei za bidhaa za vyakula.




Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Kipindi	2022	2023	2024	2025	2026
Jan	207,899	124,736	270,984	646,480	567,469
Feb	203,297	106,881	326,172	619,659	560,008
Mac	200,626	80,123	336,099	587,062	533,634
Apr	190,366	63,808	340,102	557,228	500,962
Mei	149,402	51,367	340,002	509,990	
Jun	141,576	46,665	340,479	477,923	
Jul	140,695	94,088	368,855	485,930	
Ago	144,410	210,020	489,187	537,571	
Sep	149,044	244,169	651,403	570,519	
Okt	151,794	244,289	708,399	593,485	
Nov	147,401	244,223	702,502	590,425	
Des	137,655	248,282	677,115	577,376	

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

Mfumuko wa bei ya nishati, mafuta na bili za maji uliongezeka kufikia asilimia 5.3 mwezi Aprili 2026, kutoka asilimia 2.1 katika mwezi uliotangulia, chini ya asilimia 7.3 ya mwezi kama huo mwaka 2025 (Jedwali 2.1.1). Ongezeko la mwezi Aprili 2026, lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa bei za mafuta nchini (Kielelezo 2.1.4), ikiashiria athari za mgogoro ya kijiipolitiki unaoendelea Mashariki ya Kati.

Kielelezo 2.1.4: Bei za Bidhaa za Mafuta




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi uliendelea kuwa na mchango mkubwa katika mfumuko wa bei wa jumla, ukichangia asilimia 2.4 mwezi Aprili 2026, juu kidogo ya mwezi uliotangulia na mwezi kama huo mwaka 2025 (Kielelezo 2.1.5).

Kielelezo 2.1.5: Mchango Katika Mfumuko wa Bei

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.


2.2 Sera ya Fedha

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC), katika kikao chake kilichofanyika mwezi Aprili 2026, iliamua kutokubadili Riba ya Benki Kuu (CBR) na kubaki asilimia 5.75 kwa robo mwaka inayoishia Juni 2026. Uamuzi huu ulilenga kudhibiti vihatarishi vya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi, wakati ambao migogoro ya kijiipolitiki imeongezeka hususan Mashariki ya Kati. Vilevile, MPC ilipunguza wigo wa Riba ya Benki Kuu kutoka asilimia 2 hadi 1.5, ikiwa na lengo la kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha.

Utekelezaji wa sera ya fedha mwezi Aprili 2026 ulikuwa wa matokeo ya kuridhisha, ikiwezesha kuwepo ukwasi wa kutosha katika sekta ya benki na kuhakikisha riba za mikopo ya muda mfupi katika soko la fedha vinaendana na mwelekeo wa sera ya fedha. Katika mwezi husika, wastani wa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki (IBCM) ulikuwa asilimia 6.15, ukiendelea kubaki ndani ya wigo wa Riba ya Benki Kuu (Kielelezo 2.2.1). Mikopo ya muda mfupi kwa benki (reverse repo) ilipungua hadi shilingi bilioni 379.7 mwezi Aprili 2026 kutoka shilingi bilioni 585.7 mwezi uliotangulia, ikiakisi kuongezeka kwa ukwasi katika sekta ya benki (Kielelezo. 2.2.2).




Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabanki



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ukuaji wa ujazi wa fedha uliendelea kuwa sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 22 mwezi Aprili 2026, karibu sawa na asilimia 23.2 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1).

Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

Kipengele	Kiasi (Shilingi Bilioni)			Ukuaji kwa mwaka (%)		
	Apr-25	Mac-26	Apr-26	Apr-25	Mac-26	Apr-26
Rasilimali halisi za nje	14,658.6	15,245.6	14,553.0	45.3	-1.3	-0.7
Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu	12,273.9	13,916.0	13,066.2	12.6	5.3	6.5
Rasilimali halisi za nje za mabanki	2,384.7	1,329.6	1,486.8	---	-40.2	-37.7
Rasilimali halisi za ndani	38,679.1	49,001.1	50,538.9	13.0	33.5	30.7
Madaai rasmi ya ndani	51,989.3	59,877.3	61,722.8	14.8	19.5	18.7
Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara	8,189.3	10,272.1	10,659.9	-3.6	27.8	30.2
Mikopo kwa sekta binafsi	38,755.8	47,216.5	47,919.3	14.8	24.3	23.6
Rasilimali nyinginezo	-13,310.2	-10,876.3	-11,183.9	20.3	-18.9	-16.0
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	53,337.7	64,246.7	65,091.9	20.3	23.2	22.0
Amana za fedha za kigeni	13,846.3	14,998.4	14,989.0	31.9	10.2	8.3
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	39,491.4	49,248.3	50,102.9	16.8	27.8	26.9
Amana zinginezo	15,478.3	19,071.4	18,951.4	14.1	27.2	22.4
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	24,013.1	30,176.9	31,151.6	18.5	28.2	29.7
Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko	7,024.1	8,078.3	8,107.1	14.3	12.4	15.4
Amana za hundi	16,989.0	22,098.5	23,044.5	20.3	35.1	35.6
Fedha za msingi (M0)	11,878.9	14,998.9	15,670.5	18.0	27.2	31.9

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kuonyesha ukuaji imara, ikiongezeka kwa asilimia 23.6 katika kipindi cha mwaka ulioishia Aprili 2026, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 24.3 uliorekodiwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.2.4 na 2.2.5).

Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.2.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabanki




Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa imara katika shughuli kuu za kiuchumi. Biashara ilirekodi ukuaji mkubwa zaidi wa asilimia 44.2, ikifuatiwa na shughuli za uchimbaji madini na mawe, pamoja na uchukuzi na mawasiliano (Jedwali 2.2.2). Wakati huo huo, mikopo kwa shughuli binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa hutumika kugharamia jasiriamali ndogo sana, ndogo na za kati iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote iliyoelekezwa kwa sekta binafsi, ikichangia asilimia 35, ikifuatiwa na shughuli za biashara na kilimo (Kielelezo 2.2.6).

Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi

	Asilimia						
	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jan-26	Feb-26	Mac-26	Apr-26
Biashara	14.4	24.1	21.3	50.0	48.7	43.3	44.2
Uchukuzi na mawasiliano	23.8	25.6	25.7	34.2	39.4	39.5	39.7
Uchimbaji Madini	-10.5	22.9	20.8	91.4	103.9	78.4	39.7
Kilimo	29.8	29.8	30.2	27.9	31.9	28.5	30.5
Ujenzi	39.2	27.9	25.7	29.5	28.1	21.8	20.6
Shughuli binafsi	14.7	13.6	13.7	17.8	18.9	20.7	17.7
Hoteli na migahawa	7.0	21.7	22.5	1.6	5.2	4.4	6.0
Viwanda	7.7	7.3	2.5	-7.7	-8.5	-4.9	4.2

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.3 Viwango vya Riba

Katika mwezi Aprili 2026, riba za mikopo na amana za benki kwa kiasi kikubwa hazikuwa na mabadiliko, zikiwa na ongezeko dogo katika riba za mikopo na amana. Wastani wa riba za mikopo uliongezeka hadi kufikia asilimia 15.33, toka asilimia 15.11 mwezi Machi 2026. Vilevile, riba za mikopo kwa wateja wakubwa (negotiated lending rates) ziliongezeka

kidogo hadi asilimia 12.56 kutoka asilimia 12.21 mwezi uliotangulia (Jedwali 2.3.1).

Wastani wa riba za amana uliongezeka kidogo hadi asilimia 8.54 kutoka asilimia 8.33 mwezi Machi 2026, huku riba za amana kwa wateja wakubwa zikipungua kidogo kufikia asilimia 11.37 kutoka asilimia 11.57. Kufuatia mwenendo huu, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.50, kutoka asilimia 5.85 mwezi Machi 2026 (Jedwali 2.3.1).

Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa Benki za Biashara

	Asilimia					
	Apr-25	Des-25	Jan-26	Feb-26	Mac-26	Apr-26
Riba za amana	2.89	3.02	2.94	2.98	2.89	2.91
Riba za mikopo - jumla	15.16	15.24	15.10	15.11	15.11	15.33
Riba za mikopo (mwaka 1)	16.15	15.46	15.49	15.41	15.45	15.31
Riba za mikopo (wateja wakubwa)	12.88	12.38	12.25	12.19	12.21	12.56
Riba za amana -jumla	7.82	8.36	8.33	8.32	8.33	8.54
Riba za amana (miezi 12)	9.27	9.58	9.70	9.82	9.60	9.81
Riba za amana (wateja wakubwa)	10.52	11.66	11.74	11.48	11.57	11.37
Tofauti kati ya riba za mikopo na amani	6.88	5.88	5.79	5.59	5.85	5.50

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

2.4 Masoko ya Fedha


Soko la dhamana za Serikali

Soko la dhamana za serikali liliendelea kufanya kazi kwa ufanisi, likichangiwa na mahitaji ya wawekezaji pamoja na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi. Mwezi Aprili, 2026, Benki Kuu ilifanya minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi zenye thamani ya shilingi bilioni 429.8 kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali na utekelezaji wa sera ya fedha.

Minada yote ilikuwa na mahitaji makubwa kuliko kiwango kilichotangazwa, ikifikia zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 859.5, ambapo shilingi bilioni 450.4 zilikubaliwa. Sanjari na mahitaji makubwa ya wawekezaji, wastani wa riba ulipungua hadi asilimia 5.06 kutoka asilimia 5.21 mwezi Machi 2026 (Kielelezo 2.4.1).



Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, Benki ilifanya minada ya hati fungani za miaka 5 na 10, zenye thamani ya Shilingi bilioni 174.9 na shilingi bilioni 144.6, mtawalia, kwa ajili ya kugharamia matumizi ya Serikali. Minada yote miwili ilikuwa na mahitaji makubwa kuliko zabuni zilizotangazwa, ikifikia zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 408.3, kati ya hizo zabuni zenye thamani ya Shilingi bilioni 291.3 zilikubaliwa. Wastani wa riba za hati fungani ulipungua hadi asilimia 9.54 kwa hati fungani ya miaka 5 na asilimia 9.40 kwa hati fungani ya miaka 10.

Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki (IBCM) liliendelea kuwezesha usambazaji wa ukwasi baina ya benki. Jumla ya mauzo katika soko yalikuwa shilingi bilioni 2,708.5 kwa mwezi Aprili 2026, ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,699.5 kwa mwezi uliotangulia. Mikopo ya siku 7 imeendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote katika soko, kwa asilimia 60.5 (Kielelezo 2.4.2). Wastani wa riba katika soko uliongezeka hadi asilimia 7.32, ikilinganishwa na asilimia 6.32 ya mwezi Machi 2026.

Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Soko la fedha za kigeni

Ukwasi wa fedha za kigeni katika soko la ubadilishaji fedha ulikuwa wa kutosha, ukichagizwa na mapato ya fedha za kigeni hususan kutokana na mauzo ya dhahabu nje ya nchi. Jumla ya mauzo katika soko ilifikia dola za Marekani milioni 64.6, ikilinganishwa na dola milioni 137.5 mwezi Machi 2026 na dola milioni 48.4 mwezi Aprili 2025 (Kielelezo 2.4.3). Benki Kuu ilishiriki sokoni kwa kuuza dola milioni 15.3 ili kudumisha utulivu wa soko.

Thamani ya Shilingi iliendelea kuwa imara dhidi ya sarafu zingine, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,612.46 kwa dola moja ya Marekani mwezi Aprili 2026, ikilinganishwa na Shilingi 2,684.41 kwa dola moja kipindi kama hicho mwaka 2025. Hii ni sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 2.68 kwa mwaka, ikilinganishwa na asilimia 2.53 mwezi uliotangulia, na kushuka kwa thamani kwa asilimia 3.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2025.

Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania




2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Mapato ya ndani ya Serikali yaliendelea kuwa ya kuridhisha, ambapo katika mwezi Machi 2026 Serikali ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 3,836.8, sawa na asilimia 8.5 juu ya lengo la mwezi husika. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 3,703.3 zilikusanywa na Serikali Kuu sawa na asilimia 96.5 ya mapato ya jumla, ikiwa juu ya lengo kwa asilimia 9.3 (Kiambatisho, Jedwali A2).

Mapato ya kodi yaliendelea kuwa imara yakifikia shilingi bilioni 3,317.5, sawa na asilimia 10.8 juu ya lengo. Hali hii inaashiria athari chanya za maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi pamoja na kuongezeka kwa uzingatiaji wa ulipaji kodi. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kodi ya mapato ambayo ilizidi lengo kwa asilimia 17.2. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 385.7, ikiwa ni asilimia 1.7 chini ya lengo la mwezi (Kielelezo 2.5.1).

Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Machi




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Serikali imeendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato, ambapo yalifikia jumla ya shilingi bilioni 4,273.4. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 2,545.3 zilitumika kugharamia matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 1,728.1 zikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Machi



Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) lilifikia dola za Marekani milioni 51,067.2 mwishoni mwa mwezi Aprili 2026, sawa na ongezeko la asilimia 0.5 kutoka kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa mwezi Machi 2026. Kati ya kiasi hicho, asilimia 70.4 ilikuwa ni deni la nje (Kiambatisho, Jedwali A10).

Deni la Nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) lilikuwa dola za Marekani milioni 35,949.6 mwishoni mwa Aprili 2026. Katika kiasi hicho, asilimia 82.7 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1). Mikopo ya nje iliyopokelewa mwezi Aprili 2026 ilikuwa dola za Marekani milioni 54, ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 242.0 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 190.4 zilitumika kufanya malipo ya mkopo mkuu.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji kwa kiasi kikubwa haukuwa na mabadiliko na ule wa mwezi Machi 2026, huku mashirika ya kifedha ya kimataifa yakibakia kuwa wakopeshaji wakuu, yakichangia asilimia 58.3 ya deni lote, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Wakati huo huo, mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za



usafirishaji na mawasiliano iliongezeka kwa asilimia 22.4, ikifuatiwa na mikopo kwa ajili ya kufadhili urari wa malipo ya nje na bajeti (BoP na budget support). Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 66.0, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya (Euro) (Jedwali 2.6.3 na Jedwali 2.6.4).

Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji

Dola za Marekani Milioni

Mkopaji	Apr-25		Mac-26 ^r		Apr-26 ^p	
	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Serikali Kuu	27,314.0	80.9	29,679.8	82.7	29,717.5	82.7
Deni ambalo halijalipwa	27,236.1	80.7	29,599.9	82.5	29,637.3	82.4
Malimbikizo ya riba	78.0	0.2	80.0	0.2	80.1	0.2
Sekta binafsi	6,446.7	19.1	6,206.3	17.3	6,232.1	17.3
Deni ambalo halijalipwa	5,853.1	17.3	5,778.4	16.1	5,785.9	16.1
Malimbikizo ya riba	593.7	1.8	427.9	1.2	446.2	1.2
Mashirika ya umma	3.8	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Deni ambalo halijalipwa	3.8	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Malimbikizo ya riba	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Jumla ya deni la nje	33,764.5	100.0	35,886.2	100.0	35,949.6	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebisha; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji

Dola za Marekani Milioni

Mkopeshaji	Apr-25		Mac-26 ^r		Apr-26 ^p	
	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Mashirika ya fedha ya kimataifa	18,965.7	56.2	20,826.5	58.0	20,950.3	58.3
Deni ambalo halijalipwa	18,931.8	56.1	20,803.3	58.0	20,926.1	58.2
Malimbikizo ya riba	33.8	0.1	23.2	0.1	24.2	0.1
Nchi washirika wa maendeleo	1,463.2	4.3	1,553.5	4.3	1,558.4	4.3
Deni ambalo halijalipwa	1,385.3	4.1	1,473.6	4.1	1,478.3	4.1
Malimbikizo ya riba	78.0	0.2	80.0	0.2	80.1	0.2
Benki za kimataifa za biashara	12,253.2	36.3	12,778.5	35.6	12,710.1	35.4
Deni ambalo halijalipwa	11,869.4	35.2	12,429.1	34.6	12,345.0	34.3
Malimbikizo ya riba	383.8	1.1	349.4	1.0	365.1	1.0
Mikopo ya mauzo ya nje	1,082.4	3.2	727.7	2.0	730.7	2.0
Deni ambalo halijalipwa	906.4	2.7	672.4	1.9	673.8	1.9
Malimbikizo ya riba	176.1	0.5	55.3	0.2	56.9	0.2
Jumla ya deni la nje	33,764.5	100.0	35,886.2	100.0	35,949.6	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebisha; na p, takwimu za awali

Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa Asilimia

Shughuli ya uchumi	Apr-25	Mac-26 ^r	Apr-26 ^p
Msaada wa urari wa malipo yote ya nje na bajeti	20.7	22.3	22.3
Usafirishaji na mawasiliano	21.5	22.3	22.4
Kilimo	5.0	5.3	5.3
Nishati na madini	12.9	12.0	12.0
Viwanda	3.5	3.7	3.7
Huduma za jamii na elimu	20.2	19.2	19.3
Fedha na bima	4.2	3.6	3.6
Utalii	1.8	1.8	1.8
Mali isiyohamishika na ujenzi	4.8	5.1	5.1
Mengineyo	5.5	4.8	4.5
Jumla	100.0	100.0	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebisha; na p, takwimu za awali

Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia

Sarafu	Apr-25	Mac-26 ^r	Apr-26 ^p
Dola ya Marekani	66.6	66.3	66.0
Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro)	17.4	17.6	17.7
Yuan ya China	6.4	6.5	6.6
Sarafu nyinginezo	9.7	9.7	9.7
Jumla	100.0	100.0	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania


Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali lilifikia Shilingi bilioni 39,335.8 mwishoni mwa mwezi Aprili 2026, ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.3 juu ya kiasi kilichorekodiwa mwishoni mwa mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.6.1). Ongezeko hilo lilitokana zaidi na matumizi makubwa ya bakaa hasi (Jedwali 2.6.5 na Jedwali 2.6.6).



Kielelezo 2.6.1: Deni la ndani la Serikali kuu



Chanzo: Wizara ya Fedha

Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

Jedwali 2.6.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo

Shilingi Bilioni

Nyenzo	Apr-25		Mac-26		Apr-26 ^p	
	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Dhamana za serikali	29,582.4	85.1	33,321.1	86.7	33,438.1	85.0
Dhamana za serikali za muda mfu	1,935.6	5.6	1,575.3	4.1	1,518.7	3.9
Hisa za serikali	187.1	0.5	135.7	0.4	135.7	0.3
Dhamana za serikali za muda mrefu	27,459.6	79.0	31,609.9	82.2	31,783.7	80.8
Vyeti vya ushuru	0.1	0.0	0.1	0.0	0.1	0.0
Deni lililo na dhamana	5,177.5	14.9	5,126.8	13.3	5,897.6	15.0
Madeni mengine ^q	18.4	0.1	0.0	0.0	0.0	0.0
Bakaa hasi	5,159.1	14.8	5,126.8	13.3	5,897.6	15.0
Deni la ndani (ukiiondoa karatasi za ukwasi)	34,759.9	100.0	38,447.9	100.0	39,335.8	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

Jedwali 2.6.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji

Shilingi Bilioni

Mkopeshaji	Apr-25		Mac-26		Apr-26 ^p	
	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)	Kiasi	Mchango (%)
Benki za bias hara	10,049.9	28.9	10,925.8	28.4	11,052.2	28.1
Benki Kuu ya Tanzania	7,119.2	20.5	6,935.5	18.0	7,706.3	19.6
Mifuko ya hifadhi ya jamii	9,171.1	26.4	10,463.9	27.2	10,426.4	26.5
Kampuni za bima	1,858.4	5.3	1,997.1	5.2	2,012.5	5.1
Mifuko maalumu ya Benki Kuu	564.5	1.6	788.4	2.1	798.4	2.0
Wengine	5,996.8	17.3	7,337.0	19.1	7,339.8	18.7
Deni la ndani (ukiiondoa karatasi za ukwasi)	34,759.9	100.0	38,447.9	100.0	39,335.8	100.0


Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na wawekezaji wasio wakazi

Katika mwezi Aprili 2026, Serikali ilikopa jumla ya Shilingi bilioni 392.3 kupitia uuzaji wa dhamana za Serikali. Kati ya kiasi hiki, Shilingi bilioni 245.1 zilikopwa kupitia uuzaji wa hati fungani za Serikali na Shilingi bilioni 147.2 kupitia uuzaji wa dhamana

za muda mfupi za Serikali (Kielelezo 2.6.2). Wakati huo huo, malipo ya deni la ndani yalikuwa jumla ya Shilingi bilioni 552.1, yakihusisha Shilingi bilioni 275.2 za malipo ya deni la msingi na Shilingi bilioni 276.9 za malipo ya riba.

Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka, ikiashiria kupungua kwa kasi ya kuimarika kwa sekta ya nje. Kwa mwaka ulioishia Aprili 2026, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilikuwa dola za Marekani milioni 2,651.8, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,107.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.7.1). Hali hii ilichangiwa zaidi na ongezeko kubwa la uagizaji wa bidhaa na huduma, ambazo zilizidi mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

Licha ya ongezeko la nakisi ya urari wa malipo ya kawaida, akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha ikifikia dola za Marekani milioni 5,722.5 mwishoni mwa mwezi Aprili 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,307.7 kipindi kama hicho 2025. Kiwango hicho kinatosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.4 ya makadirio ya uagizaji, na hivyo kubaki juu ya lengo la kitaifa na la Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kielelezo 2.7.1).




Jedwali 2.7.1: Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali

Dola za Marekani Milioni

	Apr-25	Mac-2026	Apr-26	Mwaka ulioishia Aprili			Mabadiliko ya asilimia
				2024	2025	2026 ^p	
Urari wa bidhaa	-461.1	-596.6	-963.3	-5,979.9	-4,553.6	-5,353.5	17.6
Zilozouzwa nje*	649.9	815.0	788.0	7,815.8	9,682.7	11,215.0	15.8
Zilizonunuliwa nje	1,111.0	1,411.6	1,751.3	13,795.7	14,236.3	16,568.5	16.4
Urari wa huduma	218.57	266.0	237.3	4,151.4	3,908.0	4,285.6	9.7
Mapato	493.8	551.9	525.8	6,466.0	6,942.3	7,661.7	10.4
Malipo	275.3	285.8	288.5	2,314.6	3,034.2	3,376.1	11.3
Urari wa bidhaa na huduma	-242.5	-330.6	-726.0	-1,828.5	-645.6	-1,067.9	65.4
Bidhaa na huduma zilozouzwa nje	1,143.8	1,366.9	1,313.8	14,281.7	16,625.0	18,876.7	13.5
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	1,386.3	1,697.5	2,039.7	16,110.2	17,270.5	19,944.6	15.5
Urari wa malipo wa vitega uchumi	-223.7	-135.0	-132.6	-1,608.4	-1,998.4	-1,852.0	-7.3
Yaliyoingia	17.5	23.9	20.1	338.5	301.8	297.7	-1.3
Yaliyotoka	241.2	158.9	152.7	1,946.9	2,300.2	2,149.7	-6.5
Urari wa uhamisho mali ya kawaida	28.9	21.2	20.2	667.8	531.9	268.1	-49.6
Iliyolingia	78.1	82.0	82.2	1,323.6	1,117.2	926.4	-17.1
ambapo Serikali	4.9	0.0	0.0	140.9	133.1	20.2	-84.8
Iliyotoka	49.2	60.8	62.0	655.8	585.3	658.3	12.5
Urari wa bidhaa, huduma na uhamisho mali	-437.3	-444.4	-838.4	-2,769.1	-2,112.1	-2,051.8	25.6

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

Mauzo ya nje

Katika mwaka ulioishia Aprili 2026, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 13.5 na kufikia Dola za Marekani milioni 18,876.7, ukuaji ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mauzo ya dhahabu nje ya nchi pamoja na mapato yatokanayo na sekta ya utalii (Kielelezo 2.7.2).


Mauzo ya bidhaa nje ya nchi ambayo yalichangia takribani asilimia 59.7 ya jumla ya mauzo ya nje, yaliongezeka hadi Dola za Marekani milioni 11,215 katika mwaka unaoishia Aprili 2026 kutoka Dola za Marekani milioni 9,682.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo ya dhahabu, bidhaa zilizotengenezwa viwandani, na mauzo ya bidhaa asilia hususan tumbaku na korosho (Kielelezo 2.7.2).

Mauzo ya dhahabu yalipanda kwa kiasi kikubwa, yakichangiwa na kuendelea kwa bei nzuri katika soko la dunia, huku ukuaji wa mauzo ya bidhaa za viwandani kwa kiasi kikubwa ulichangiwa na chuma, vioo na nguo. Vilevile ongezeko la mauzo ya bidhaa asilia kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na hali nzuri ya mauzo katika soko la dunia.

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya nje ya bidhaa yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 788 mwezi Aprili 2026 kutoka dola za Marekani milioni 649.9 mwezi Aprili 2025, kwa kiasi kikubwa yakichangiwa na dhahabu, na bidhaa za viwandani.

Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma

Dola za Marekani Milioni



Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali


Mapato yatokanayo na utalii, yalichangia asilimia 57 ya mapato ya jumla ya huduma, huku yakiendelea kuwa mchangiaji mkuu wa huduma, na kurekodi ukuaji wa mwaka wa asilimia 10.4 hadi kufikia dola za Marekani milioni 7,661.7 kwa mwaka unaoishia mwezi Aprili 2026 (Kielelezo 2.7.3). Mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 9.5 hadi dola za Marekani milioni 4,385.3 yakiakisi ongezeko la wageni wa kimataifa waliowasili, hadi 2,281,340 kutoka 2,162,487 katika mwaka ulioishia Aprili 2025. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mapato ya huduma yalifikia dola



za Marekani milioni 525.8 mwezi Aprili 2026, juu zaidi ya dola za Marekani milioni 493.8 mwezi Aprili 2025.

Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta

Dola za Marekani Milioni



Chanzo: Ukurutoaji wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

Uagizaji wa bidhaa na huduma

